


Haki ya Msingi ya Usawa mbele ya Sheria.

TAWLA ipo kwa kukusaidia wewe kuelewa nini hasa maana ya Haki hii.

Endapo una swali lolote, au unahitaji msaada, tafadhali tuandikie "TAWLA", S.L.P. 9460, Dar es Salaam Tanzania.



DESIGN NA MICHORO WALTER LEMA
(DESIGN AND DRAWING)
REDISIGN HELMUT PFINDEL

IMEFADHILIWA KWA PAMOJA
NA ROYAL DANISH EMBASSY
IMEFADHILIWA NA MEDICAL MISSION SUPPORT
UNITED STATES INFORMATION SERVICES (USIS)

UKATILI WA KIJINSIA



IMETOLEWA NA KUTAYARISHWA NA CHAMA CHA
WANAWA KE WANASHERIA TANZANIA (TAWLA)

MAANA YAKE NINI

Ni unyanyasaji na ukatili unaofanywa dhidi ya wanawake na baadhi ya wanaume na jamii ambao humdhalilisha mwanamke kimawazo, kisiasa, kiuchumi na kijamii na matokeo yake mwanamke kukosa uhuru, maendeleo na utu wake.

UNATENDEKA DHIDI YA NANI

Unatendeka dhidi ya wanawake wa rika zote.

KWA NINI

1. Kutokana na baadhi ya mila na desturi.
2. Uwezo mdogo wa kiuchumi.
3. Elimu duni.
4. Kutojamini kwa wanawake.
5. Mazoea.
6. Dharau za wanaume.
7. Misimamo mibovu ya ndoa.
8. Heshima inayotokana na hofu.
9. Wazazi kutoa upendeleo kwa watoto, wanaume.
10. Baadhi ya Sheria za dinj na za Serikali.
11. Tabia za kinyama.

MADHARA YAKE NI YAPI

1. Maumivu, machungu simanzi na huzuni katika familia
2. Magonjwa yasiyoweza kutibika.
3. Ulemavu.

4. Kuvunjika kwa ndoa/uchumba.
5. Watoto wa mitaani.
6. Chuki kati ya familia/koo.
7. Maumbile ya kike kuharibiwa.
8. Kutoaminiana kati ya wanawake na wanaume
9. Wanawake kutoshiriki pamoja na wanaume katika shughuli za maendeleo.
10. Vifo.
11. Wanawake wakiwa ni asilimia kubwa ya wananchi, maendeleo ya nchi yanarudi nyuma.

JAMII IFANYE NINI

1. Kuwe na Sheria nzuti na kali kulinda haki za wanawake.
2. Serikali jhakikishe mikataba ya Kimataifa ya haki za binadamu zinapitishwa kama sheria za nchi.
3. Wanawake wapewe nafasi ya kufanya maamuzi kuhusu elimu na afya zao n.k.
4. Wanawake wapewe nafasi ya kuelewa na kutawala miili yao.
5. Wanawake wapewe haki ya usawa katika jamii, Serikali, vyombo vya Sheria na familia zao.
6. Kazi zinazofanywa na wanawake zitambuliwe.
7. Wanawake wapatiwe elimu sawa sawa na wanaume na hivyo kupewa nafasi sawa katika kazi.
8. Wanawake waweze kuamua matumizi ya kipato chao na cha familia.
9. Wanawake wawe na haki ya kurithi na kumiliki mali.

10. Jamii iwape moyo wa kujitambua na kujiamini.
11. Wanawake wasinyanyaswe kimapenzi.
12. Sheria ziwe kali dhidi ya makosa ya unyanyasaji wanawake na watoto.
13. Wanawake na wanaume washirikiane katika kutetea haki za wanawake.

SHERIA INASEMAJE

1. Katiba inatamka wazi kuwa:
 - Binadamu wote huzaliwa huru, na wote ni sawa.
 - Kila mtu anastahili heshima ya kutambuliwa na kuthaminiwa utu wake.
2. Ni kosa la jinal kufanya shambulio la aibu dhidi ya mwanamke.
3. Ni kosa la jinai kumdhalilisha kijinsia, kumbaka kumlawiti mwanamke.
4. Ni kosa la jinai kumdhalilisha, kumtishia. kumsababishia madhara ya kimwili au kumpiga mwanamke nakadhalika.

WANAWAKE WAFANYEJE?

Mapambano ni makali - vitendo vya namna hii vitolewe taarifa mara vinapotokea.